JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za simu

Mkuu wa shule: 0755 853 233/0787 947 141

Makamu Mkuu wa Shule: 0765 293 955

Matron: 0755275056

Shule ya Sekondari Kizwite,

S.L.P. 215, Sumbawanga,

Tarehe ……...

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …….

S.L.P. ……..

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIZWITE HALMASHAURI YA MANISPAA SUMBAWANGA MKOA WA RUKWA MWAKA 2022/2023.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka **2022/2023** tahasusi ya **HGL/HKL/CBG/PCB**. Shule ya Sekondari Kizwite ipo umbali wa kilometa 3 Kusini mwa mji wa Sumbawanga mjini.Usafiri wa basi kutoka mjini kuelekea shuleni unapatikana katika kituo cha mabasi stendi kuu soko matola au soko kuu nauli ni shilingi 500/= bajaji ,shilingi 2,000/= bodaboda na tax ni shilingi 5,000/= au 4,000/= hii ni hasa kwa wale wanaotokea barabara ya Mpanda. Kwa wale wanaotokea barabara ya Mbeya washukie Stendi ya Kizwite ni karibu sana na shule, kwa bodaboda ni Tshs 1,000/= tu.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe **…….** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **…….** Mwisho wa kuripoti ni tarehe……...

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

2.1 Sare ya shule

a) Sare ya shule hii ni mashati mawili (2) meupe mikono mirefu, sketi mbili(2) rangi *ya ugoro(brown colour) na nyeusi.* (Rangi ya Vitambaa imeambatanishwa ni vya suti estim namba moja) Mshono wa sketi; mshono wa linda box kubwa mbele na nyuma na malinda mawili kushoto na mawili kulia. (**NB**: Sketi ziwe ndefu zifike kwenye **viatu**,sketi fupi hazihitajiki zitakaguliwa. Maelezo ya mshono. *(Angalia picha ukurasa wa 8).***NB***:**Kama rangi za skirt na shamba dress zinakusumbua /zinakuchanganya usishone ,bali ukifika shuleni utapewa maelekezo na kushona ukiwa shuleni.*

b) . **Kwa wanafunzi Waislamu** aje na hijab (kijuba) nne (4) , mbili (2) ziwe nyeupe na mbili (2) ziwe bluu bahari zote ziwe na urefu na upana wa wastani.

c). Sare ya michezo kwa shule hii ni Tracksuit moja rangi ya bluu bahari,,raba pea moja nyeusi,bukta ya bluu na T- shirt bluu.

d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi vinavyo ziba mguu.

e) Soksi jozi mbili (2) nyeupe.

f) Sweta moja (1) *rangi ya zambarau yenye shingo (V) lisilo na vifungo*

g) Nguo za kushindia gauni(*shamba dress*) mbili *(2) kunguru draft yenye rangi nyeupe na nyeusi, mshono wa solo.Angalia picha ukurasa wa 8)*

h) Tai ndefu mbili (2) *rangi nyeusi na ugoro.*

i) Kwa ajili ya baridi mwezi juni na,julai,aje na kaba shingo(pull neck) rangi nyeusi na jacketi nyeusi.

2.0 Ada na Michango ya shule.

a) **Ada ya shule** kwa mwaka ni shilingi 70,000/=. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja.

b) **Michango** inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

i) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
ii) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma.
iii) Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
iv) Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza .
v) Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa).
vi) Mtihani wa kujipima wa kidato cha tano =Tshs 20,000/=

Jumla ya Ada na Michango tu ni Tshs.170,000/= kwa Mwaka na nusu muhula ni Tshs.135,000/=.

Ada na Michango hiyo hapo juu ilipwe katika Benki ya NMB akaunti Namba 62102300007 (*Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip). Jina la akaunti:Kizwite Secondary School.* Isipokuwa *kitambulisho na picha na Nembo ya shule fedha italipwa taslimu shuleni kwa mhasibu.*

NB:*Fedha zote ikiwa ni Ada ya shule na Michango ya shule zilipwe kuanzia (mwezi wa saba) tarehe 1St Julai 2022.*

c) **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

i) Ream ya karatasi-1 **A**4 (kwa mwaka)
ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa ukurasa wa 9).
iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia.
iv) Scientific calculator kwa wanafunzi wa Sayansi.
v) Godoro Ft 2½ x 6. au Shillingi 10,000/= kukodisha godoro kwa muhula,lakini siyo lazima unaweza kuja nalo.
vi) Mashuka pair-2 rangi ya pink, blanketi-1 rangi yoyote, foronya-1 rangi ya pink, chandarua 1 rangi yoyote ,
vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
viii) Ndoo mbili(2) ndogo-1 na kubwa-1 zenye mifuniko.
ix) Kwanja-1,Hard broom-1(mfagio wa dukani mgumu wa kusugulia sakafu),Ruber squizer au Drier 1(kwa ajili ya kukaushia maji) na mfagio mmoja (1) wa chelewa
x) Aje na kitenge /kanga au taulo kwaajili ya kuogea
xi) Masanduku (tranka)/mabegi makubwa hayaruhusiwi, kwani hatuna nafasi ya kuyatunza. Akija nalo atalazimika kurudisha kwa gharama zake.
xii) Aje na cheti cha kuzaliwa au kiapo cha mahakamani (Affidavit) na Result slip ya kidato cha Nne.Vyote viwe ni nakala (Copy).

NB: **a).**Kutokana na umuhimu na gharama za **matibabu** tunashauri kuwa kama mwanafunzi ana bima ya afya aje nayo na kama hana mzazi au mlezi unashauriwa umkatie bima ya afya.

b).**Fedha za kuja nazo shuleni taslimu (Cash)** ni:- Ths 6,000/= kitambulisho,Tshs 2,000/= Nembo na Tshs 10,000/= kwaajili ya kukodisha Godoro.

3. Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu **Na.25** ya mwaka**1978** na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria **Na.10** ya mwaka**1995**.Aidha,inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
i) Kutunza mali ya umma.

4. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro.
iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv) Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzake, mwalimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v) Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
vi) Kusuka mwenye kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
vii) Kufuga ndevu.
viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix) Uvutaji wa sigara.
x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi) Kudharau bendera ya Taifa.
xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

5. **Baadhi tu ya kanuni za shule**:Ni marufuku tena ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kutenda yafuatayo:-

a. Kuwa bwenini wakati wa vipindi (**adhabu yake ni kurudishwa nyumbani**)

b. Kuwa na nywele fupi haturuhusu kusuka. **Hivyo ni lazima kunyoa nywele .**

c. Kuwa na kucha ndefu ama kuzipaka rangi,kupaka wanja rangi ya midomo , kuvaa hereni,bangili,pete, kofia ,mzura na mapambo mengine yoyote hayaruhusiwi kabisa.

d. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

NB: Kama mwanao hawezi kuishi bila simu ya mkononi, basi hafai katika mazingira ya shule ya sekondari Kizwite na ni vema asifike kabisa shuleni maana atafukuzwa shule mara moja. Hivyo mawasiliano yote yatafanyika kupitia namba zifuatazo:

Mkuu wa shule: 0755 853 233/0787 947 141, Makamu Mkuu wa Shule: 0765 293 955,Mwalimu wa Nidhamu 0752476080 na Matron: 0755275056. **Mwanafunzi haruhusiwi kutumia simu nyingine nje ya hizo.**

Ni matumaini yangu kuwa mzazi/mlezi wako atashirikiana nasi katika kukuongoza hadi ufanikiwe kuipata elimu ya sekondari ya juu ipasavyo.

6. **Viambatanisho na fomu Muhimu.**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.*(Jaza kisha ilete shuleni)*

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.(*Jaza kisha ilete shuleni)*

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. .(*Jaza kisha ilete shuleni.*

d) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

7. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

P. G. NZWALILA

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIZWITE
SUMBAWANGA

Fomu Na 1

SUMBAWANGA MUNICIPAL COUNCIL

KIZWITE SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 215,
SUMBAWANGA – RUKWA

MEDICAL OFFICER,
……..

…….

RE: MEDICAL EXAMINATION:

MR/MISS: …….

Please examine the above named pupil as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this School. The examination should include the following categories

1. Hemoglobin …….
2. P.V. Bleeding ……..
3. Sight ……..
4. Blood pressure ……..
5. Urine for Sugar and Pregnancy……
6. Stool for routine examination ……..
7. Asthma ……..
8. Skin/Diseases ……..
9. Leprosy ……..
10. Pulmonary tuberculosis……..
11. Neurosis ……..
12. Venereal diseases ……..
13. Other serious diseases ……..

PART B:

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

1. I have examined the above named pupil and Consider that he/she is Physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full schooling.
2. Other comments: …….
   ……..

DATE:…… ……

SIGNATURE AND OFFICIAL STAMP

NB: (Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)

FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI
A:TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi(kama alivyo andikisha kwenye mtihani wa kidato cha nne)
……..
2. Kabila……3.Dini……4.Dhehebu……
5. Tarehe ya kuzaliwa…… 6. Mahali alipozaliwa …… 7. Uraia……

8. Shule ya sekondari alipomaliza kidato cha Nne ……

B:TAARIFA ZA MZAZI /MLEZI

Picha

1. Jina kamili la baba ……Hai/amefariki
3. Jina kamili la mama …… Hai/amefariki
   Kazi ya baba……
   Kazi ya mama……

Picha

4. Anwani ya baba……..…
   Anwani ya mama
……..

Picha

5. Jina kamili la Mlezi…….
   Kazi ya mlezi……..
   Simu ……
6. Utakuwa unakwenda wapi wakati wa likizo?.....

(Wakati wa likizo unatakiwa kwenda kwa mzazi au mlezi aliyetajwa tu. Kama utabadilisha mahali pa kwenda likizo, mzazi/mlezi atoe idhini kwa maandishi mwezi mmoja kabla)

7. Taja ndugu wawili (2) na wazazi /walezi wawili (2) wanaoweza kuja kukuona shuleni. Bandika picha (Passport size) zao hapa chini, na uhusiano na mawasiliano yao.

1. Jina …… ……. …
   Uhusiano…… ……
   Sehemu anayoishi……

Picha

   Namba ya simu……

2. Jina……..
   Uhusiano……
   Sehemu anayoishi……

Picha

   Namba ya simu……..

8. Maelezo mafupi kuhusu afya ya mwnafunzi……
9. Ninathibitisha kwamba taarifa zilizotolewa hapo juu ni kamili na sahihi.
   Jina la mzazi/mlezi……
   Sahihi ya mzazi/mlezi ……Tarehe ……

NB: (Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)

Fomu Na:3

MKATABA/ AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi…… (jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii.

Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote. Nafahamu kwamba kitendo che kilicho kinyume na mwenendo na taratibu za shule kinastahili adhabu kali hata kufukuzwa shule kama itakavyo amuriwa na jumuiya pamoja na baraza la ushauri la shule.

Saini ya mwanafunzi…….

Tarehe……..…

Shahidi

Jina kamili……..

Saini…….

Tarehe……..

AHADI YA MZAZI:

Mimi…… ……..(jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi

wa……..…..…..Kidato cha……mwaka……..…….

Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule .Pia naahidi kumlipia ada na michango yote iliyoagizwa kwenye maelekezo ya kujiunga na shule hii.

Saini ya Mzazi/Mlezi…….

Anuani kamili…….

Simu:……

Tarehe:…….

NB: (Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)

MFANO WA RANGI YA SKETI YA UGORO (BROWN COLOUR) NA SHAMBA DRESS **Fomu Na:4**



Rangi ya kitambaa cha ugoro

Rangi ya kitambaa cha shamba dress

MFANO WA GAUNI (SHAMBA DRESS)



VITABU VYA TAHASUSI:-

Kwa sababu shule ina uhaba wa vitabu, ikiwezekana ni vizuri aje na vitabu vitakavyomsaidia kwa masomo husika kati ya vilivyoorodheshwa hapa chini:-

I. VITABU VYA KEMIA:-

1. BY S. chand, Conceptual Chemistry for class XI and XII
2. By Tanzania Institute of Education, ADVANCED LEVEL INORGANIC CHEMISTRY part I and II.
3. Advanced chemistry riview (2000 -2012)

II. VITABU VYA BIOLOJIA:-

1. By Taylor at el (1999) Biological Science, third edition. Tong printing press Hong kong.
2. By Glenn and Tod,s (1999) Understanding Biology 4th Ed.Stanlye Thomes Ltd UK.

III. VITABU VYA HISTORY:-

1. By Webster J.B. The Growth of African Civilization, the Revolutionary Years of West Africa Siche 1800, Longman Press.
2. By Walter Rodney, How Europe Underdeveloped Africa.

VI. VITABU VYA JIOGRAFIA:-

1. Pritchard J.M. (1979), Africa a study Geography for Advanced students London Longman. ritchard J.M. (1979), Africa a study Geography for Advanced students London Longman. 2. Msabila D. T (2003) Success in Geography climatology and Soil Science Dar es salaam – Afroplus Industries L.T.D
3. Prichard J.M. (1990) practical Geography for Africa Longman.
4. Kamili, 2, physical Geography for Africa Dar es salaam Afroplus Industries.
5. Msabila D.T. Physical Geography Dar es slaam Nyambari Nyangwine Publishers.
6. Msabila D.T. (2006) Human and economic Geography (Advanced level paper 2) Nyambai Nyangwine publishers.

VII. VITABU VYA LANGUAGE(1) ONE:-

1. Nichlolus arshery, Comprehensive English Grammar New edition.
2. Michael Kadeghe, Sematics phonology and styhstics. (blue)
3. Advanced level English ,Apractical Approach By Nicholous Ashel
4. EnglishText book for Advanced Level By Kadeghe Michael

VIII. LANGUAGE (II) TWO NOVELS:-

1. Lyi Kwei Armal, The beautiful one are not yet born
2. Chunua Achebe, A man of the people
3. PLAYS
4. Heinrich Ibsen, An Enemy of the people
5. Ngungi wa Thiongo, I will merry when I want.
6. Advanced level Literature By Nyambari Nyangwine and Godfrey Rutta Bukagile

IX. GENERAL STUDIES:-

General studies Approach

X. PHYSICS BOOKS:

1. Principle of Physics for Class XI By S .Chand
2. Principle of Physics for Class XII By S .Chand
3. Advanced Physics 7th edition by Nelkon and Parker.
4. Understanding Physics.
5. Rodger Manchester.
6. Calculation for A-Level

XI. VITABU VYA KISWAHILI:-

1. J.A.MASEBO na M.Nyangwine, Nadharia ya Kiswahili Kidato cha Tano na Sita.
2. H. J.M. Mwasiko, R.D.K. Mekacha, D.L. Masoko, P.C.K. Mtengwa; Kitanglizi cha Tafsiri Nadharia na Mbinu.
3. Tahakiki kidato cha tano na sita.
4. Nadharia ya Fasihi kidato cha tano na sita Kiswahili II.
5. Kiswahili – I: Mwandishi Masuko Christopher Saluhaya.
6. Kitangulizi cha Tafsiri, Nadharia na Mbinu. Wandishi:- H.J.M. Mwansoko, R.D.K. Makacha, S.L.W. Masoko, P.C.K. Mtengwa